

Serikali yataka chanjo ugonjwa unaosumbua kwato za ng'ombe

Yasema mwaka ujao wa fedha chanjo hiyo lazima ipatikane

Bakari Kiango, Mwanaranchi
bkiango@mwanaranchi.co.tz

Dar es Salaam. Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel ametaka Wakala wa Maabara ya Vetinari Tanzania (TVLA), kuhakikisha chanjo ya ugonjwa wa mdomo na miguu unaosumbua ng'ombe inapatikana mwaka wa fedha ujao.

Ng'ombe akipata ugonjwa huo huwa anatoka vidonda kwenye mdomo na miguuni kwenye eneo la kwato.

Profesa Ole Gabriel alisema hayo juzi, wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa baraza la wafanyakazi uliofanyika Dar es Salaam.

Profesa Ole Gabriel alisema ni wakati mwafaka sasa kwa taasisi hiyo kuhakikisha chanjo

NUKUU

"Tafadhalini sana fanyeni linalowezezana, sisi tutatoa ushirikiano popote mtakapokwama. Tukipata chanjo hii (ng'ombe) tutapata masoko makubwa ya mifugo pamoja kuluza nje ya nchi."

Profesa Elisante Ole Gabriel

hizo zinapatikana, huku akimtaka mtendaji wa TVLA kufanya kila linalowezezana ili mchakato huo ufanikiwe.

"Wafungie wataalamu popote pale au wasafiri kwenda nje ya nchi lakini mwaka ujao wa fedha chanjo ipatikane. Ofisi yangu itakupa ushirikiano katika ngazi zote, tunataka wafugaji nchini watambue jambo hili linakuja," alisema Profesa Ole Gabriel.

Aliwataka watumishi wa TVLA kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika taasisi hiyo.

Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk Stellah Bitanyi alisema miongoni mwa mipango ya taasisi hiyo ni kuongeza chanjo ya saba ya homa ya mapafu ya mbuzi.

Dk Bitanyi alisema wanakusudia kuzalisha chanjo dhidi ya homa ya mapafu ya ng'ombe kwa kuagiza mashine kubwa ya kugandisha chanjo vichupa 2,000 kwa wakati mmoja.

Alisema lengo ni kuongeza uzalishaji wa chanjo hiyo ili kukidhi mahitaji makubwa ya soko la ndani ya nchi.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini, Profesa Hezron Nonga alisema TVLA ina jukumu la kuchunguza magonjwa ya mifugo pamoja na kufanya utafiti.

Alisema inachunguza na ufuatiliaji wa udhhibiti ubora wa viuatilifu.

MAELEKEZO: TUNAELEKEA HUKU

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Ellsante Ole Gabriel akizungumza wakati wa uzinduzi wa baraza la wafanyakazi wa Wakala wa Maabara ya Vetinari Tanzania (TVLA) uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam. Picha na Loveness Benard

